JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA

HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHE. DKT. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

NOVEMBA 6, 2023

1.0 UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

2. ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

3. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nimpongeze kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa uongozi wake mahiri wa kuwatumikia watanzania. Aidha, ninatambua umahiri wake katika kusimamia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali ili kuboresha huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Vilevile, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa busara, hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu. Kadhalika, nampongeza **Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa mbunge wa jimbo la Ruangwa - Lindi**, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na Kiongozi wa shughuli za Serikali bungeni, kwa uongozi wake hodari na kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali. Nitumie fursa hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb)** kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati.

4. ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi, kwa kuchaguliwa kuwa **Rais wa 31 wa mabunge duniani (Inter Parliamentary Union)** na **Rais wa kwanza mwanamke kutoka Bara la Afrika na Tanzania** kushika wadhifa huo. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi duniani wanayo juu ya nchi yetu na wewe mwenyewe. Aidha, napenda kukupongeza tena wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa umahiri na

kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Vilevile, ninawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya **Mwenyekiti** wake **Mheshimiwa Sillo Daniel Baran, Mbunge wa Babati Vijijini** (**CCM**) na **Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi** (**CCM**) kwa maoni na ushauri wakati wa vikao vya Kamati. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 ninayowasilisha katika Bunge hili leo.

6. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Naibu Waziri wa Fedha**, **Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb),** na watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na **Katibu Mkuu**, **Dkt. Natu El-maamry Mwamba** kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii, vitabu vya mapendekezo ya Mwongozo pamoja na utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru sana Wizara, Taasisi, Idara za Serikali, Sekta Binafsi na wadau mbalimbali waliotoa maoni na michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mwongozo huu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 ni ya tatu kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Mwongozo umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu ya Mwaka 2020, malengo ya kimkakati ya mwaka 2020 (Strategic Development Goals - SDGs 2030), maelekezo mengine ya Serikali na Agenda ya Afrika 2063. Vilevile, mapendekezo haya yamezingatia mafanikio, changamoto na fursa zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mwongozo wa mwaka 2023/24 na Bajeti ya mwaka 2022/23.

8. ***Mheshimiwa Spika***, mapendekezo haya yanaakisi juhudi ambazo Serikali ya awamu ya sita inachukua katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuendelea: kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kutoa fursa za ajira;

kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini; kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wote; kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kimataifa; kuweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji na viwanda; pamoja na kudumisha amani, usalama, utawala bora, umoja na utulivu nchini. Mapendekezo yanayowasilishwa yameainisha masuala muhimu ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa Mipango na Bajeti za mafungu yao ili kufikia malengo yaliyobainishwa katika vipaumbele vya Taifa.

9. ***Mheshimiwa Spika***, mapendekezo haya yameainisha masuala mbalimbali, ikiwemo: mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25; usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti; mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2022/23; mapitio ya utekelezaji wa mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24; na maelekezo yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti kwa mwaka 2024/25.

2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

2.1 Mwenendo wa Viashiria vya Uchumi

10. ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na changamoto zilizojitokeza na kuathiri uchumi wa dunia, uchumi wa Tanzania uliendelea kuimarika kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita ikiwemo utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine; na utoaji wa ruzuku ya mbolea na mafuta ya petroli. Uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 4.7 kwa mwaka 2022, na unatarajiwa kuongezeka hadi asilimia 5.2 mwaka 2023 na asilimia 5.8 mwaka 2024. Aidha, kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2023, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.3 ikilinganishwa na asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Pamoja na mambo mengine, ukuaji wa uchumi ni matokeo ya uwekezaji wa kimkakati wa Serikali katika miundombinu ya nishati, usafirishaji na huduma za kijamii, kuongezeka kwa uzalishaji wa madini na shughuli za utalii. Shughuli za kiuchumi zilizochangia kwa sehemu kubwa katika ukuaji huo ni kilimo, ujenzi na uchimbaji wa madini.

11. ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.6 katika mwaka ulioishia Juni 2023 ambao ulibakia ndani ya lengo la nchi na

mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Aidha, mfumuko wa bei kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

12. ***Mheshimiwa Spika***, mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 kwa mwaka 2022/23 ikilinganishwa na lengo la ukuaji la asilimia 10.7. Ukuaji huo umeongezeka ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 mwaka 2021/22. Ukuaji huu unaakisi ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la UVIKO–19; jitihada zinazoendelea kutekelezwa na Serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti. Aidha, mikopo chechefu ilipungua kufikia wastani wa asilimia 5.3 Juni 2023 kutoka asilimia 7.8 Juni 2022.

13. ***Mheshimiwa Spika***, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi. Hadi kufikia Juni 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa dola za Marekani bilioni 5.45 ikilinganishwa na dola bilioni 5.11 Juni 2022. Kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9. Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi 4.0 na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

14. ***Mheshimiwa Spika***, hadi Juni 2023, Deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 82,137.9. Mikopo hii imetumika kugharamia miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2022 inaonesha kuwa deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

15. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2022/23, kampuni za Moody's Investors Service Ltd na Fitch Rating Services Ltd zilifanya tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka (Credit Rating) na kuchapisha matokeo ya daraja B2+ na B+, mtawalia. Matokeo haya yanaashiria kuimarika kwa hali ya uchumi, usimamizi wa deni na uwekezaji pamoja na hatua ya Serikali ya awamu ya sita katika kufungua shughuli za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Aidha, tathmini hii itaiwezesha nchi kutambulika zaidi katika masoko ya fedha ya kimataifa na hivyo kuongeza sifa za kuvutia uwekezaji na kupanua wigo wa kupata mikopo kwa Serikali na sekta binafsi.

16. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1 cha Mwongozo**.

2.2 Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23

17. ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2022/23, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 41,480.6. Hadi Juni 2023, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 38,977.0 sawa na asilimia 94.0 ya lengo. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 26,277.9 mapato ya ndani sawa na asilimia 93.8 ya lengo la mwaka; shilingi bilioni 3,562.9 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 76.6 ya lengo; na shilingi bilioni 9,136.2 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi sawa na asilimia 103.7 ya lengo. Aidha, Serikali imetumia shilingi bilioni 40,853.3 kugharamia utekelezaji wa bajeti. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 26,882.6 zilitumika kugharamia deni la Serikali, mishahara ya watumishi na uendeshaji wa shughuli za Serikali; na shilingi bilioni 13,970.7 ziligharamia programu na miradi ya maendeleo.

18. ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/23 yanajumuisha: ugharamiaji wa shughuli za Serikali; miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR), Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya afya, elimu, maji, barabara na viwanja vya ndege; ulipaji wa mishahara; na deni la Serikali kwa wakati.

19. ***Mheshimiwa Spika***, changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2022/23 ni pamoja na: kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali ikiwemo bidhaa za petroli, mbolea na chakula kutokana na athari za vita kati ya Urusi na Ukraine; kudorora kwa uchumi wa dunia hususan katika masoko ya fedha; uwepo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kodi kwa kuingiza bidhaa nchini kupitia njia mbalimbali za udanganyifu ikiwemo magendo; mwitikio mdogo wa kutoa na kudai stakabadhi za kielektroniki za EFD wakati wa mauzo; na mabadiliko ya tabianchi.

20. ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kukabiliana na changamoto zilizoainishwa hapo juu ni pamoja na: kutoa ruzuku kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa za petroli na bei ya

mbolea ili kupunguza gharama za uzalishaji na kudhibiti mfumuko wa bei; kuendelea kuboresha sheria za kodi, uwekezaji pamoja na biashara; kuimarisha mifumo ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato; kuimarisha doria maeneo ya mipakani; kutoa elimu kwa walipa kodi kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa hiari na matumizi ya stakabadhi za kielektroniki za EFD; kuanzisha tuzo za uzalendo kupitia mfumo wa risiti za kielektroniki (EFD) inayotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni; na kuendelea kusimamia sera za bajeti na fedha.

21. ***Mheshimiwa Spika***, fursa zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa bajeti inajumuisha: ongezeko la mahitaji ya chakula katika soko la dunia; kuongezeka kwa soko la ndani kutokana na ongezeko la idadi ya watu; uwepo wa nguvu kazi kubwa ya Taifa ambayo ni vijana; ukuaji wa miji ambao umekuwa ukifungua fursa nyingi za kiuchumi; ufanisi mdogo katika matumizi ya faida ya jiografia ya nchi kuhudumia nchi za EAC na SADC; uwepo wa amani, umoja na utulivu wa uchumi; ongezeko la bei ya vito vya thamani katika soko la dunia; uwepo wa vyumba vichache vya kuhudumia watalii ikilinganishwa na ongezeko la idadi ya watalii; na mahitaji ya viwanda vya ndani kutokana na kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujenga uwezo wa ndani wa kutumia rasilimali zilizopo ikiwemo ardhi, misitu, gesi asilia, madini, vyanzo vya maji (bahari, mito na maziwa), nguvu kazi, idadi ya watu, jiografia ya nchi, amani na utulivu na Mkongo wa Taifa ili kuongeza shughuli za uzalishaji wa bidhaa na huduma.

22. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2023/24, mapato yaliyokusanywa katika vyanzo vyote ni shilingi bilioni 9,163.5. Kati ya mapato hayo, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 6,878.9, sawa na asilimia 95.2 ya lengo la shilingi bilioni 7,224.0. Ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa shilingi bilioni 10,437.7.

23. ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2022/23 yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1** cha Mwongozo.

3.0 MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2024/25

24. ***Mheshimiwa Spika***, misingi iliyotumika katika kuandaa shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye

shughuli za uwekezaji na biashara; kuendelea kuhimili athari za majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko, mafuriko); kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; kuendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuendelea kuimarika kwa utoshelevu wa chakula nchini; na uwepo wa amani, usalama, utawala bora, umoja, utulivu wa ndani na nchi jirani.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa ni pamoja na:

(i) Pato Halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.2 mwaka 2023 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2024;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 3.0 hadi 7.0 katika kipindi cha muda wa kati;

(iii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.4 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2024/25 kutoka uwiano halisi wa asilimia 11.9 uliofikiwa mwaka 2022/23;

(iv) Nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) kuwa asilimia 2.2 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 2.7 ya mwaka 2023/24;

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(vi) Kuimarika kwa viashiria vya ustawi wa jamii.

3.1 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25

26. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 47,424.9. Mapato ya ndani yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 34,436.2, sawa na asilimia 72.6 ya bajeti yote. Aidha, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi bilioni 4,291.9, sawa na asilimia 9.0 ya bajeti. Serikali inatarajia kukopa shilingi bilioni 6,141.9 kutoka soko la ndani na shilingi bilioni 2,555.0 kutoka soko la nje. Maoteo ya Bajeti ya Serikali ya mwaka 2024/25 yamezingatia mwenendo wa ukusanyaji mapato, matarajio ya ukuaji wa uchumi, hali ya uchumi wa dunia pamoja na mikakati ambayo Serikali inaendelea kuchukua katika kuongeza mapato ya ndani kama ilivyoainishwa kwenye **Sehemu ya Pili ya Mwongozo**.

27. ***Mheshimiwa Spika***, matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 47,424.9 mwaka 2024/25. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali shilingi bilioni 12,101.2, mishahara shilingi bilioni 11,774.8 na uendeshaji wa shughuli

za Serikali shilingi bilioni 8,223.8. Aidha, matumizi kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 15,325.1 ikijumuisha ruzuku ya maendeleo (Elimumsingi na Sekondari bila ada na Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu). Makadirio haya yamezingatia mahitaji ya kugharamia deni la Serikali; mishahara ya watumishi wa umma; uendeshaji wa miradi iliyokamilika ikiwemo miundombinu ya elimu, afya, umeme na maji; ugharamiaji wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa; na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

28. ***Mheshimiwa Spika***, baadhi ya mikakati itakayotumika katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani ni pamoja na kuendelea: kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha vyanzo hivyo vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato; kuhakikisha taasisi zenye sura za utoaji wa huduma kwa pamoja ikiwemo vituo vya utoaji wa huduma kwa pamoja (one stop center) vilivyopo vinaboresha mifumo ya ukusanyaji kwa kuwezesha kutoa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali; kuweka sera/mikakati ya kuchochea uchumi unaotumia miamala ya kielektroniki ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu (cash - lite economy); kuwarasimisha wafanyabiashara na watoa huduma wadogo kwa kuwatengea maeneo maalum na kuwapatia huduma muhimu za kijamii kwa lengo la kukuza biashara zao; na kuanzisha tuzo za uzalendo kupitia mfumo wa risiti za kielektroniki (EFD).

29. ***Mheshimiwa Spika***, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2024/25 umeainishwa katika **Sehemu ya Pili ya Mwongozo**.

3.2 Maelekezo Mahsusi ya Mwongozo

30. ***Mheshimiwa Spika***, Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wakati wa uandaaji, utekelezaji, na ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti. Miongoni mwa maelekezo hayo ni kama ifuatavyo:

3.2.1 Uandaaji

(i) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa wakati wa utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25 hakutakuwa na bajeti ya nyongeza ambayo itatengwa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za fungu ambazo hazikutengewa bajeti;

(ii) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutoa kipaumbele katika kutenga bajeti ya kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya;

(iii) Maafisa Masuuli waratibu na kushiriki vikao vya Kamati za Bajeti za Mafungu;

(iv) Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwa na mikakati ya kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika Mafungu wanayosimamia;

(v) Kutenga bajeti kwa ajili ya kugharamia majukumu ya msingi ya mafungu ili kuepuka uhamisho wa fedha usio wa lazima na uzalishaji wa madeni. Baadhi ya maeneo mangine ya kuzingatia ni kutenga bajeti kwa ajili ya: **miradi inayoendelea**; mchango wa Serikali (counterpart fund) katika miradi yenye masharti hayo inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo; kugharamia shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2024; kugharamia shughuli za ushirikiano na kuimarisha Muungano; na kulipa fidia katika maeneo ya utekelezaji wa miradi;

(vi) Wizara za kisekta kutojumuisha bajeti za shughuli za mafungu ya Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenye mafungu yao kwa kazi zinazotekelezwa na mafungu hayo. Aidha, kwa shughuli zinazotegemeana, Mafungu yapange kwa pamoja (coordinated planning);

(vii) Kuzingatia Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 kinachoelekeza kutoingia mikataba na Washirika wa Maendeleo ya kupokea misaada na mikopo pasipo idhini ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya Fedha;

(viii) Kuainisha vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti pamoja na mikakati ya kukabiliana navyo;

(ix) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 kwa kuweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa makandarasi na wazabuni wasio wakaazi nchini ili kuwawezesha wale ambao ni wakaazi nchini (local content) na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi. Aidha, kuhakikisha makubaliano yote (Financing Agreement) na Washirika wa Maendeleo katika miradi mikubwa yanazingatia

ushirikishaji wa wazawa usiopungua asilimia 30 ya gharama ya mradi; na

(x) Kutekeleza miradi yenye mvuto wa kibiashara kwa utaratibu wa kushirikisha sekta binafsi (PPP) ili kupunguza gharama zinazoweza kuepukika kwenye bajeti ya Serikali.

3.2.2 Utekelezaji

(i) Kuzingatia Mwongozo Kuhusu Maombi na Utoaji wa Fedha za Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali wa mwaka 2021 unaosisitiza kutoingia mikataba bila kuwa na maandalizi ya msingi na bajeti ya shughuli husika;

(ii) Kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(iii) Kuwezesha utoaji wa namba ya malipo jumuishi ili kurahisisha ulipaji kodi, ada na tozo mbalimbali kwa wateja na hivyo kuongeza uhiari wa ulipaji wa mapato ya Serikali;

(iv) Kuhakikisha mikataba mipya inayoingiwa inatumia shilingi ya Tanzania kwa lengo la kupunguza uhitaji wa matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima;

(v) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (NeST) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi; na

(vi) Kuhakikisha taasisi za kibiashara na za kimkakati zinazingatia Waraka wa Msajili wa Hazina Na.1 wa mwaka 2023, katika kuimarisha mfumo wa usimamizi na utendaji kazi.

3.2.3 Ufuatiliaji na Tathmini

(i) Kuhakikisha kunakuwa na mpango shirikishi wa ufuatiliaji na tathmini kwa kuwajumuisha wadau wote muhimu wa ndani ya taasisi au taasisi nyingine ili kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

(ii) Kuandaa viashiria vya kupima utekelezaji wa malengo ili viwe vipimio vya mafanikio ya taasisi au mradi husika;

(iii) Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa mpango na bajeti unaakisi malengo, shabaha na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; na

(iv) Kuhakikisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinafuatilia uzingatiwaji wa Sheria ya Bajeti kuhusu utendaji wa Kamati ya Bajeti kwa lengo la

kupitia na kujadili taarifa za ufuatiliaji, tathmini na utekelezaji kila robo mwaka ili kuleta uwajibikaji.

4.0 ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahsusi ya Mwongozo yanapatikana katika **Sehemu ya Nne ya Mwongozo.**

5.0 HITIMISHO

31. ***Mheshimiwa Spika***, mapendekezo ya Mwongozo yatawezesha kukamilika kwa maandalizi ya Bajeti za Mafungu kwa wakati; kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarika kwa utawala bora na utawala wa sheria; na kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti. Hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 sambamba na Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake.

32. ***Mheshimiwa Spika*****,** baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

33. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb)
W.F
06 Novemba 2023